

Jenga Brand Yako

Mwongozo wa Kujenga Brand
Binafsi na Brand ya Biashara

Fidelis Butondo

Jenga Brand Yako

Mwongozo wa Kujenga Brand
Binafsi na Brand ya Biashara

Fidelis Butondo

Simu: +255(0) 738 132 250

Barua pepe:

Fbutondo@gmail.com

Instagram: fidelisbutondo

ISBN 97-9912-40-074-0

Haki zote zimehifadhiwa, hivyo hairuhusiwi mtu ye yote kunakili, kurudufisha au kuhifadhi kwa njia ya kielekitroniki au njia yo yote kitabu chote au sehemu ya kitabu hiki bila ruhusa ya maandishi kutoka kwa mwandishi wa kitabu hiki.

Yaliyomo

UTANGULIZI	iv
SHUKRANI	vii
Kuhusu Brand/Chapa	1
Maana ya Brand/Chapa.....	10
Nguvu ya Mtandao	29
Wewe ni Brand.....	42
Namna ya kujenga brand ya biashara	50
Jina la biashara	76
Bobeza katika jambo moja	84
Brand kama dini	90

UTANGULIZI

Mtazamo chanya ni moja ya kitu pekee ambacho katika maisha mimi na wewe tunakihitaji kwani vitapelekea maisha yenye mafanikio na furaha, ili uweze kuwa na furaha unahitaji mtazamo chanya katika fikra zako, na unapotaka kufanikiwa unahitaji kutengeneza mtazamo chanya katika fikra za wengine.

Hii inatokana na uhalisia kuwa huwezi kufanikiwa kwa kujitegemea wewe mwenyewe, unahitaji watu ili waweze kukufanikisha na kukufikisha unakotaka kwenda.

Kwa mtazamo huo huo hauwezi ukafanya mauzo yeyote pasipo watu kuamua kama watanunua kwako ama la! Hii ni kwa mauzo yako binafsi au mauzo ya kampuni.

Ndio maana liko hitaji la kutengeneza chapa (brand) ili uwape watu sababu ya kwanini wanunue kutoka kwako, iwe unajiuza kwa ajili ya mahojiano (interview) ya kazi au mauzo ya bidhaa.

Dunia ya sasa imejaa kelele! nina maana kuwa kila kitu sasa kinafanana sio bidhaa tu zilizopo sokoni bali hata watu wanafanya vitu kwa kuigana kitu kinachopelekea mtu

kushindwa kufanya chaguzi sahihi. Wanafunzi wanamaliza na sifa zinazofanana, viwango vya ufaulu (GPA) za kufanana n.k. Iko haja kubwa ya kujitofautisha na wengine na njia pekee ya kujitofautisha ni kupitia chapa (brand) zetu.

Kitabu unachokisoma kitakusaidia kuijenga chapa yako kwani kila mtu anayo ya kwake. Kwa kufahamu chapa zetu tutaweza kujitofautisha na wengine na kuvutia mafanikio yetu binafsi na katika biashara zetu.

Kwa upande wa biashara vilevile changamoto bado ni kubwa kwani tuna biashara nyingi zinaanzishwa sababu tu mwingine anafanya biashara kama hiyo, hivyo tunajikuta tuna biashara na bidhaa nyingi sokoni ambazo hazidumu.

Kampuni nyingi zimekuwa zikizalisha bidhaa tu na sio chapa/brand, kitu ambacho mshindani wako anaweza akazalisha pia, ama akachukua biashara yako na kukupoteza sokoni kwa kupunguza bei tu, maana wote mna bidhaa ile ile.

Ni wakati ambao kampuni na biashara inabidi zizalishe chapa na sio bidhaa, kwani kuna utofauti mkubwa kati ya bidhaa na chapa

- Bidhaa inatengenezwa kiwandani

- Brand inatengenezwa kwa mahusiano na uaminifu kwa wateja
- Bidhaa ni rahisi kuigwa na mshindani wako.
- Brand ni ya tofauti na ya ubunifu
- Bidhaa ni rahisi kupitwa na wakati
- Brand ni ya kudumu

